



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**  
**WIZARA YA AFYA**  
**TAARIFA KWA UMMA**

**MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 16/04/2020.**

Wizara ya Afya, Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya sita (6) wa Corona (COVID-19) nchini na kufikia idadi ya wagonjwa 24 kutoka 18 ambao tuliowatolea taarifa tarehe 15 Aprili 2020. Taarifa za wagonjwa wapya wa ni kama ifuatavyo;

1. Mwanamme, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 30, mkaazi wa Kibweni
2. Mwanamme, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 27, mkaazi wa Magogoni
3. Mwanamme, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 28, mkaazi wa Kwarara
4. Mwanamke, Mtaanzania, mwenye umri wa miaka 58, mkaazi wa Kilimahewa juu.
5. Mwanamme, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 23, mkaazi wa Amani
6. Mwanamme, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 55, mkaazi wa Kidoti

Wagonjwa wote ni Raia wa Tanzania hawana historia ya kusafiri nje ya nchi siku za hivi karibuni. Wagonjwa wote wamelazwa katika vituo maalum kwa ajili ya kuendelea na matibabu.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo kunawa mikono kwa maji yakutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuhairisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima.

Wizara inaomba wananchi ambao wana dalili za homa kali, kukohowa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya afya au kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyo husiana na ugonjwa huu.

Aidha katika kipindi hichi tunawataka wananchi wale wanaofikwa na misiba wachukuwe tahadhari jinsi ya kuwashughulikia, kuwakafini na kuwazika maiti, na tunawashauri ni vyema washirikiane na wataalamu wetu wa afya kwa kupata miongozo stahiki.

Ndugu wananchi tuendeele kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kululinda na kutuepusha na maradhi haya.

Hamad Rashid Mohamed (MBM, MBLW)

Waziri wa Afya -Zanzibar